Visisimizi Muhimu

Wakati wa mikutano, warsha au kongamano za mafunzo, mara kwa mara nguvu za watu waliohudhuria hudidimia na kuonekana wachovu. Hali kama hii yaweza kushuhudiwa nyakati za asubuhi, baada ya maakuli ya mchana au jioni kabisa. Kuwasilisha miswada ngumu, joto jingi na mijadala yenye changamoto yaweza kurahisishwa iwapo kuna mapumziko.

Jambo lolote la kichekesho au la kusisimua watu hujulikana kama visisimizi. Visisimizi hivi huchangia mengi mbali na kuamsha watu waliohudhuria mkutano. Visisimizi huchangia katika kujifahamisha na wenzako waliohudhuria vikao. Husaidia katika kuondoa vikwazo na kuleta pamoja watu kutoka kwa tabaka mbalimbali. Kuna aina mbalimbali ya visisimizi-na watu wanaweza kubuni wenyewe.

Unapochagua kisisimuzi, chagua kwa uangalifu na makini, huku ukizingatia hadhi ya watu walio hudhuria. Iwapo watu hao hawana ufahamu wa visisimuzi, anza na vile vilivyo rahisi. Daima jiunge nao ili kuonyesha mfano. Heshimu wale wasiotaka kushiriki. Jaribu sana kuzingatia itikadi, jinsia na ulemavu, hasa iwapo ni katika hali ambayo wanaume na wanawake watashikana. Iwapo kuna walemavu au watu wasioweza kushiriki, wachague kama waamuzi au wapatanishi. Jaribu kuchochea kisisimuzi kinacholingana na mada ya mjadala.

Vuma Uliza washiriki kugeukia wenzao na kuongea kuhusu jambo ambalo limekwisha jadiliwa, au mada ambayo imezuka, ajenda au mkataba uliafikiwa.

Tarakimu Simama katika duara. Hesabu kwa zamu katika duara. Kila baada ya kufika nambari ya tano, mhusika apige makofi badala ya kuitikia tarakimu hiyo. Kila baada ya kufika tarakimu ya saba, mhusika anazunguka pasipo kusema tarakimu hiyo. Iwapo mhusika atakosea, yeyote anayemkaribia ataanza kuhesabu upya.

Kusonga, Kama kiongozi songa kwingineko. Kusonga katika eneo lingine kutasababisha watu kugeuza vichwa au kusongesha viti na kuamka. Ni bora kualika watu kusimama na kukaribia picha au chati.

Buni makundi Uliza wahusika kubuni makundi ili kujadili kuhusu mada au jambo fulani. Wahusika wanaweza kubuni makundi ya watu watatu, wanne au watano. Waweza kuhesabu watu (`Moja, mbili, tatu, moja...'), au kuwauliza kuandaa makundi pamoja na watu ambao hawajuani, kutoka kwa shirika au kundi lingine.

Kuchukua nafasi Uliza wahusika kujichagulia nafasi katika kisisimuzi ili kuwasilisha ujumbe fulani. Unaweza kueleza wahusika kuchukua nafasi na kuonyesha mchezo kuhusu mafunzo ya kitamaduni, matatizo yake na faida katika kuwasilisha ujumbe. Wahusika kama hao wanaweza kuigiza vipengele fulani vya kitamaduni, au hata nafasi muhimu kama kuweka hazina au kumbukumbu. Watu wapaswa kuhimizwa kuchukua nafasi katika mchezo kama huo kwani hatimaye hufaulu! Watu watafurahi katika kujianda na kutazama wenzao wakishiriki.

Nyimbo Kuimba nyimbo zilizo rahisi kujifunza ni jambo la kufurahisha. Nyimbo zilizo na viashirio hufaa, au nyimbo za kupiga makofi au kupiga dawati hufaa.

Kio Weka watu kwa makundi ya wawili. Mtu mmoja ni mhusika huku mwingine ni kama kio. Kio hufanya kila kitu kinachofanywa na mhusika, kwa kurudia ishara zote. Baada ya muda kidogo, badilishana.

Kuandika Uliza wahusika kujifanya kama kwamba wanaandika majina yao hewani kwa kutumia sehemu mbalimbali za mwili. Kama vile:

- Kidole cha kulia
- Kidole cha kushoto
- Kiwiko cha mkono wa kulia
- Kidole kikubwa
- Mabega
- Mapua

Jaribu kumaliza na kitovu!

Sauti hii ni ya nini? Mtu mmoja anatoa sauti huku wenzake wakijaribu kutambua - Yeyote anayetambua sahihi anatoa sauti nyingine. Sauti zaweza kuwa za wanyama, ndege, mashine, magari au matayarisho ya chakula.

Kusonga kwa yeyote aliye na ... Kaa katika mduara huku mtu mmoja akiwa katikati. Sema: `Yeyote aliye na .....'

- `walio valia chochote cha rangi ya samawati
- `wanaoweza kuongea lugha mbili au zaidi'
- `walio amka kabla ya saa kumi na mbili asubuhi'
- `walitumia yai, mkate, tunda n.k kama kiamsha kinywa'
- `wako na herufi s katika majina yao'... n.k

Wahusika wote (hata yule aliye katikati) watasonga katika nafasi iliyoachwa wazi na mwingine. Mtu aliye katikati ndiye anayetoa kipengele kingine.

Mvua ya kiasi Toa sauti kama ya mvua, kwa kuanza kwa taratibu, ukiendelea zaidi na kisha kuacha kwa taratibu. Uliza kila mmoja kujiunga nawe katika kuigiza mvua kwa kupiga kiganja kwa kidole kimoja cha mkono mwingine; kisha vidole viwili, tatu, nne na hatimaye mkono wote, kisha kurudi hadi kidole kimoja.

Gari moshi Uliza wahusika kuigiza sauti ya gari moshi kwa ishara za mkono. Waelekeze kwenye safari, kwa kuongeza kasi katika eneo la bonde, kuenda polepole katika mwinuko, kutia breki katika stesheni na kupunguza kasi na kuanza tena. Husisha safari hii kwa kutumia majina ya vituo maarufu.

Daraja Mtu mmoja anachagua kitu kimoja cha kuweka wengine katika vyeo au daraja. Hii yaweza kuwa kutokana na rangi ya vyatu au kiasi, nambari ya vifunguo, umri, rangi ya nywele au urefu, urefu wao, idadi ya mifuko, herufi ya kwanza ya jina au tarehe ya kuzaliwa, n.k. Buni makundi kulingana na daraja au vyeo hivyo. Kwa mfano iwapo ulichagua idadi ya vifunguo, kundi moja laweza kuwa na mtu aliye na nguo ya vifunguo vingi, na upande mwingine watu walio na nguo zisizo na vifunguo. Utahitajika kuwa mwangalifu ili usiingilie siri, kwa mfano iwapo ni vyatu, usitazame sana miguu kila mara!

Idadi kubwa ya visisimizi hivi ni kutoka kwa kitabu cha Participatory Workshops *na Robert Chambers na kunukuliwa kwa ruhusa. Kitabu hicho kimerejelewa upya katika ukurasa wa 14*

This page was last updated on 23 February 2005

Tafsiri Desemba 2006